

Komesheni dhuluma dhidi ya watoto

Serikali za ulimwengu zimekubaliana kuwa dhuluma ipo.

Inafaa tuchukue hatua haraka iwezekanavyo!

Vipi?

Serikali ni sharti:

- Zithihirishie kujitolea kwao katika kupigana vita vya dhuluma dhidi ya watoto na mata-rajio ya baadaye ambayo itaweza kuonyesha maendeleo.
- Kuunda sheria na sera ambazo zitalinda utaratibu wa haki na masilahi ya mtoto kuishi huru kutokana na dhuluma pamoja na ulinzi – aidha nyumbani, shuleni, pahali pa kazi, jamii hata kwenye taasisi.

Lini?

- Serikali za ulimwengu zinatarajiwa kuku-tana jijini New York mwishoni mwa mwaka wa 2006 ili kujadili suala la dhuluma dhidi ya watoto kwa kina. Tumia nafasi hiyo kueleza jitihada zako.

Kwa nini suala hili?

- Kwa sababu ni asilimia ishirini na nne (24%) pekee ya watoto duniani ambayo imepata ulinzi wa haki sawa na watu wa-zima. Zaidi ya mataifa 90 kote ulimwenguni bado hayajaondoa adhabu ya kuchapwa

katika shule, ingawaje mataifa mengine 30 yakiruhusu utumizi wa fimbo ama viboko kama hukumu kwenye mahakama.

- Kuna zaidi ya watoto milioni moja katika magereza na jela mbalimbali duniani ambao wananyanyaswa na kufanyiwa dhuluma kila uchao na maafisa wa magereza na wa-fungwa wenzao. Gereza ni mahali pasipofaa pa kurekebisha kwa mahitaji ya watoto q
- Kupuuza ukweli wa dhuluma za kijinsia na kugandamizwa kwa watoto ndio tatizo kub-wa zaidi – waathiriwa wakiwa watoto wa kike na makiume hudhulumiwa kimapenzi na huwa vigumu kwao kupata matibabu pamoja na haki zao kama inavyostahili. Hata wakifichua na kuthibitisha kudhulumiwa ma-hakamani, kidole cha lawama huelekezewa kidole cha lawama na kuhukumiwa.
- Watoto – wataalamu katika maisha yao wenyewe – kamwe hawahusishwi wala kupewa uhuru katika kuunda sera, mikakati au sheria zitakazolinda na kuhakikisha haki zao hazikiukwi pamoja na kujiamulia mambo yao binafsi kutoka kwa dhuluma.

Kwa habari zaidi wasiliana nasi kupitia tuvuti: <http://ecaf.savethechildren.se>



Save the Children

Ni nini kinacho hitajika?

Sera na Mikakati Maalum ya Itakayotumiwa Kulinda Haki za Mtoto na Kukomesha Dhuluma Dhidi ya Watoto

“Kulinda haki za watoto si jukumu la serikali pekee, bali ni jukumu la kila mtu kufanya hivyo.”

Maud de Boer-Buquicchio, Makamu wa Katibu Mkuu, Baraza la Ulaya

Serikali Yako Inafaa Kufanya Nini?

- Kuunda sheria ya amri ya kukomesha aina zote za dhuluma dhidi ya watoto, ikiwemo adhabu ya kudhulumu na kunyanysa watoto kimapenzi au kijinsia, kuwatumia, kuwachapa na namna zingine za kuwagandamiza au kuwavunjia hadhi/heshima.
- Kuanzisha mfumo wa kitaifa wa kulinda haki za mtoto, utakaoangazia kwa kina aina zote za dhuluma. Kwa mfano, kampeini za elimu na njia za mawasiliano na utoaji wa matumishi yanayopendelea mtoto ya kisheria, tiba na maono ya kijamii.
- Kuusisha watoto katika kufanya maamuzi muhimu pamoja na kuunda sheria na sera zao wenyewe.

- Kupunguza idadi ya watoto wanaofikishwa mahakamani, na badala yake kuanzisha mahakama maalumu za watoto zitakazo ambatana na sheria za watoto za kuwawezesha kuishi maisha ya kawaida na kuwaweka mbali na matendo ya uvunjaji wa sheria pamoja na uzuliwaji.
- Kufanya jitihada za kuwahusisha wasichana kwa wavulana katika kupigana vita vya kukomesha dhuluma dhidi ya watoto na kuwepo kwa usawa wa jinsia miongoni mwao.
- Kuunga mkono kuteuliwa kwa Mwakilishi Maalumu wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliye na uwezo wa kuendesha masharti ya kukomesha kabisa dhuluma dhidi ya watoto.

Kwa habari zaidi wasiliana nasi kupitia tuvuti: <http://ecaf.savethechildren.se>